https://dspace.org/

# Mchakato wa Uandishi Bunifu kama Unavyoakisiwa katika Riwaya za Kisasa za K.W. Wamitila

**Janice M. Mutua; Issa Mwamzandi; AbdulRahim Taib**

**2021**
Mwanga wa Lugha, 6(2), 15-26.
https://ir-library.kabianga.ac.ke/handle/123456789/1202
Mutua, J. M., Mwamzandi, I., & Taib, A. (2021). Mchakato wa Uandishi Bunifu kama Unavyoakisiwa katika Riwaya za Kisasa za KW Wamitila. Mwanga wa Lugha, 6(2), 15-26.

Downloaded from a DSpace repository. https://dspace.org/

# Mchakato wa Uandishi Bunifu kama Unavyoakisiwa katika Riwaya za Kisasa za K.W. Wamitila

*Janice M. Mutua[1], Issa Mwamzandi[2] na AbdulRahim Taib[1]*
[1]*Chuo Kikuu cha Egerton*
[2]*Chuo Kikuu cha Kabianga*

**Ikisiri**

**Makala hayaimejibana katika ufafanuzi wa upekee wa mtunzi wa riwaya za Kiswahili za kisasa pamoja na changamoto anazopitia mikononi mwa wahariri na wachapishaji kama inavyopendekezwa katika riwaya zenyewe. Aidha, makala imependekeza njia za kuboresha na kukuza riwaya mpya za Kiswahili. Madhumuni yake ni kufafanua mchakato mzima wa uandishi wa riwaya mpya kwa kuwaangazia wahusika watatu muhimu yaani mwandishi, msomaji na mchapishaji. Nadharia ya usasaleo imeuongoza mjadala huu katika ukusanyaji na uchanganuzi wa data. Mintarafu ya nadharia, mtunzi wa kazi bunifu ana uhuru wa kuandika jinsi apendavyo, hailazimu kwamba riwaya zifuate utaratibu mahususi. Mkabala wa uchanganuzi wa yaliyomo ulitumika kuchanganua data iliyohusiana na swala zima la ubunifu na uchapishaji wa riwaya mpya ya Kiswahili. Data ilichanganuliwa kwa kuangazia maudhui na vipengele vya mbinu za kimajaribio kama vile dayolojia, urejeleomatini, simulizi fupi na taashira. Riwaya za *Mwandishi, Msomaji na Mchapishajii* na *Musaleo!* zimetumika kuangazia mchakato huu. Matokeo yamewasilishwa kwa njia ya maelezo. Imebainika kuwa sura na ubunifu wa riwaya mpya ni zao la usomi. Ili kuelewa ujumbe katika riwaya za kisasa ni muhimu kwa 'mhariri' kufanya utafiti wa kina kabla ya kutoa mapendekezo yake kwa mchapishaji. Aidha, inailazimu hadhira kuwa na ufahamu wa mambo mengi kiada ili kung'amua yanayowasilishwa katika riwaya za kisasa.**

**Maneno Muhimu:** *Kariha, Riwaya za Kisasa, Mwandishi, Uandishi bunifu, Mhariri, Mchapishaji.*

**Utangulizi**

Makala hayaimezingatia shughuli zote za mtunzi wa riwaya za kisasa za Kiswahili na uandishi wake kama ilivyorekodiwa katika riwaya zilizoteuliwa. Riwaya zinatoa mwito wa kipekee kuhusu uandishi wa riwaya pamoja na kubainisha changamoto wanazokumbana nazo waandishi wa kisasa hasa pale kazi zao zinapopitia mikononi mwa wahariri na wachapishaji. Aidha, zimeonyesha baadhi ya mapendekezo yatakayoboresha na kukuza riwaya za kisasa. Lengo kuu la kufanya hivyo lilikuwa ni kupambanua nafasi za mwandishi, mhariri na mchapishaji katika mchakato mzima wa uandishi na uchapishaji wa riwaya mpya kama unavyoakisiwa katika riwaya teule za K.W.Wamitila.

Mabadiliko ya kiutunzi yaliyoshuhudiwa yamemchora mtunzi wa riwaya mpya kama mwanajamii anayetumia mbinu zisizozoeleka katika kuwasilisha ujumbe mwafaka kwa hadhira. Mabadiliko ya kiubunifu yaliyoshuhudiwa yanawiana na taswira kamili ya jamii ya kisasa inayopendelea kufanya mambo pasi na kufuata utaratibu maalum kwa mfano, miundo na mitindo tofauti ya utunzi iliyotumika na kutapakazwa kote katika riwaya. Japo mwandishi anatekeleza jukumu lake la kuiwasilisha taswira kamili ya jamii katika uandishi, mtafaruku baina yake kwa upande mmoja na msomaji na mchapishaji kwa upande mwingine unatishia kuiangamiza tajriba yake. Riwaya zilizochunguzwa zinathibitisha kuwa mtunzi wa riwaya za kisasa si mtunzi tu bali ni binadamu mwenye uwezo na mwito wa kipekee. Zinaulinganisha utunzi wake na jambo linaloibua hisia kali ndani ya nafsi yake; kariha ya utunzi. Katika makala hayaistilahi riwaya za kisasa, riwaya za kimajaribio na riwaya mpya ya Kiswahili zina maana sawa. Aidha, istilahi uandishi imerejelewa pia kama utunzi huku msomaji akirejelewa kama mhariri.

**Mwandishi kama Mwanajamii na Kariha ya Uandishi**

Katika sehemu hii, makala inamwangazia mtunzi kama mshikadau mkuu katika swala zima la uandishi bunifu. Aidha, matatizo ambayo yameukumba uandishi bunifu wa kisasa kama mwito wa kipekee wenye hisia kali yamefafanuliwa. Hususani, sehemu hii imeangazia ule mwito wa kipekee ambao humsibu mtunzi wa kisasa pindi anapojipata katika changamoto zinazomkosesha amani na matumaini ya kuendelea. Changamoto hizo huwa njia ya pekee ya kubainisha ukweli kuhusu jamii kama inavyoakisiwa na msimulizi wa riwaya ya *Musaleo!* pale anaposema:

> "Kariha yake ya kuandika humjia nyakati kama hizi anapokuwa amezongwa na hali kama hizi **(ML. UK. 34)."**

Hali zinazorejelewa za kukataliwa kwa mswada wa mwandishi aliouwasilisha kwa minajili ya kuchapishwa zinamtia kiwewe. Kwa kuwa kila mtunzi bunifu wa fasihi ana uwezo wa kujiangamiza au kujijenga (Gallop, 2011), mwandishi anaamua kuwa japo kuna vihunzi vinavyozuia uchapishaji wa kazi yake, kamwe hatanaswa na vihunzi hivyo. Riwaya zinabaini kwamba badala yake, kadri vihunzi vinavyokuwa vikali hamu ya kuandika humjaa pomoni. Riwaya teule zinasisitiza kuwa uandishi kama mwito wa kipekee huimarika zaidi wakati mambo yanapokuwa magumu. mwandishi hupata msukumo na nguvu zaidi za kuandika hali zinapomwia ngumu. Riwaya zinazidi kuhimiza kuwa kukataliwa kwa mswada si mwisho wa uandishi. Ari na motisha ya uandishi haiwezi kuzimwa na changamoto za aina yoyote ile. Aidha, katika upekee wa uandishi, maswala ya kindani yanayoibua hisia kali kuhusu uandishi na uchapishaji wa riwaya za kisasa yanaibuliwa. Imedhihirika kwamba huku wahariri na wachapishaji wakiuchukulia uandishi bunifu kama kitega uchumi mwandishi anauenzi kama jambo linalofikiriwa kwa umakini na kuwasilishwa kwa ustadi. Mintarafu ya haya, kuzidi kuandika katikati ya magumu ni mbinu moja ya kuwahimiza waandishi chipukizi kwamba wasikate tamaa.

Burke (1992) anadai kuwa mtunzi ni binadamu wa kisasa aliyejengwa na jamii. Anaendelea kufafanua kwamba mtunzi huyo anaweza kutenganishwa na nafsi yake lakini kamwe hawezi kutenganishwa na jamii. Kwa mujibu wa haya riwaya za kisasa zimebaini kuwa kama mwanajamii na binadamu mwenye wito wa kipekee, mtunzi ana uwezo wa kuchora taswira kamili ya jamii anamoishi kupitia uandishi wake. Hivyo, uandishi unafanyika kuwa kariha. Istilahi kariha inarejelea ile ari na kani inayomshika mtunzi hadi akawa na dukuduku la kutaka kuieleza jamii yake katika tajriba yake ya kiutunzi. Ni mfano wa donge linalomkaa rohoni na ambalo ghafla hupata njia aula ya kuelezewa kupitia kazi ya kifasihi atakayoitunga. Ni sawa na donge linalosakama kooni, lazima litoke ili mtu apumue! Kariha, kwa utaratibu huo, ni nguvu zinazomsukuma katika mustakabali wa uandishi wake. Hata hivyo, si kila binadamu humiliki zihi hii. Riwaya ya *Mwandishi, Msomaji na Mchapishaji* inathibitisha haya kwa kusema:

> …kila mwandishi huwa na kariha ya utunzi...kitu fulani ambacho huwa ni kama utambi unaowasha mshumaa wake wa utunzi. Nadhani Aristotle alikiita *divine afflatus…* Alisema bila hicho mtunzi hawezi kutunga. Ukijaribu utababaisha tu! **(MMM, UK. 17).**

Jibu hili la mwandishi (mhusika) katika mjadala baina yake pamoja na msomaji na mchapishaji linaeleza kilichomchochea kuandika hadithi yake jinsi alivyoiandika. Kutokana na usimulizi huu mwandishi anajitetea kuwa uandishi wake si jambo la kawaida bali ni mwito ambao hata yeye binafsi hakuuelewa. Kwa mujibu wa msimulizi wa riwaya inadhihirisha kwamba uandishi unaotokana na msukumo uliojawa na sauti nyingi zisizomaizika ndio unaodumu, mwingine utababaisha tu. Riwaya zimependekeza kuwa kazi ya mtunzi ichukuliwe kama matokeo ya uvumbuzi wa sauti ambazo haziwezi kuhusishwa na uvumbuzi wowote mahususi, ila ubunifu wa kipekee wenye nguvu za kiungu. Wazo hili linatiliwa mkazo na Burke (1995) anaposema, hisia za kuandika zinapompata mwandishi huwa hawezi kuzizuia wala kuzipuuza. Inambidi ayaandike yaliyo akilini mwake katika muundo na mtindo wowote anaouona sawa katika kuwasilishia ujumbe wake. Uwezo wa kutunga unajitokeza pale mwandishi anapowaumba wahusika na kuwaweka katika hali zinazosadikisha kile anachosimulia.

Akimrejelea Aristotle, msimulizi wa MMM anarudia wazo la uandishi kama msukumo wa ndani unaoitwa "*divine afflatus.*" Neno hili la Kilatini linamaanisha nguvu zilizomo ndani ya mwanadamu zinazomsukuma katika kutekeleza jambo fulani. Kulingana na riwaya, ni dhahiri kuwa ndani ya mtunzi mna nguvu zinazompa msukumo usioweza kusitishwa. Msukumo na upekee wake husababisha kazi za fasihi zenye mantiki (Wilson, 2004). Aidha, dhana hii imerudiwa katika riwaya ya *Musaleo!* tunapoambiwa yafuatayo:

> Kwa kweli sina. Ninachojua tu ni kwamba hamna mwandishi mwenye akili timamu. Zamani nilifundishwa kuwa wanapoandika wanajiwa na kitu kilichoitwa *Divine Afflatus*, kitu kama wazimu hivi tuseme! **(ML. UK.133)**

Mawazo sawa na hayo yanajitokeza katika riwaya ya MMM tunapoelezwa kuwa:

> Wataalamu wa fasihi wanasema kuwa huwezi kuandika wala hakuna mwandishi aliyewahi kufanya hivyo pasi na kuupata msukumo huo. Kitu fulani kinachowasha! **(MMM UK. 17)**.

Nadharia ya kiutunzi ya Aristotle inayorejelewa kwenye dondoo hili inaelekea kutusisitizia kuwa mtunzi hupatwa na hali ya uendawazimu inayomfanya abuni kazi ambayo hata yeye mwenyewe hawezi kubaini namna alivyoibuni. Huwa amepagawa na hali hiyo inapomkumba, uwezo fulani wa kiungu humjia na kumfanya kutunga kazi yake. Swala la kariha linaungana moja kwa moja na dhana ya Aristotle kuhusu ubunifu ili kuufanya uandishi bunifu kuwa tukio lake moja kuu.

Freud na Strachey (2010) wanafafanua kuwa hisia za kiroho na kiakili zina misingi katika mivurugo ya kumbukumbu kwenye sehemu za nafsi zisizoeleweka vizuri na mtu mwenyewe. Mivurugo hiyo hujidhihirisha katika ndoto za binadamu. Mintarafu ya haya riwaya zimebaini kuwa riwaya za kisasa ni matokeo ya ndoto aliyo nayo mtunzi bunifu kuhusiana na kazi yake. Kuhusu haya riwaya zinasema:

> Ninaota siku moja kuiandika riwaya. Na sio riwaya tu lakini riwaya mahususi ambayo haitakaa tu isomwe bali itasaidia usomaji wake **(ML. UK.2).**

Mwandishi anadai kuwa angependa kuiandika riwaya mpya ambayo ingejisoma yenyewe. Taashira *"Kujisoma yenyewe"* inadhihirisha kwamba hadithi husika ni kioo halisi cha jamii inayorejelewa. Mwandishi anasema kuwa hadithi atakayoitunga itaitwa *Musaleo*. Huu ni ufupisho wa *"Musa wa leo"* yaani mkombozi wa leo. Katika dini ya Kikristo iliyorekodiwa katika Biblia kitabu cha *Kutoka*, Musa alikuwa mkombozi wa wana wa Israeli kutoka utumwani Misri walikotumikishwa na Firauni. Urejeleomatini huu unabainisha kuwa baadhi ya mataifa ya Kiafrika yanayoendelea yanahitaji mkombozi wa kuyatoa katika utumwa wa maovu yanayoyakumba kama vile mauaji na ufisadi unaosababishwa na matumizi mabaya ya mamlaka. Mintarafu ya haya, riwaya itajisoma yenyewe kwa kuibaini taswira ya jamii ya kisasa, matatizo yake na mapendekezo kuhusu ukombozi wake. Aidha, inatarajiwa kuwa "Musa wa leo" ataikomboa jamii kutokana na uongozi dhalimu. Kwa mujibu huu nguvu za kipekee zilizomo katika uandishi zinampa mwandishi uwezo wa kuisawiri jamii jinsi ilivyo, kuonyesha matatizo yake na kupendekeza mbinu za kupata suluhu. Hivyo mtunzi amechorwa kama chombo cha mawasiliano. Kupitia kwa uandishi wake, utendakazi wa kawaida unaendelezwa ambapo uwezo mkubwa wa uandishi unapitishwa. Maelezo haya yanawiana na maoni ya Halliwell (1992) anaposema kwamba uwezo wa kuwa na mhemuko wa ubunifu wenye nguvu hutokana na kile anachokitambulisha kama mwongozo wa kiungu. Mintarafu ya haya, kazi ya mtunzi ni zoezi la kiakili na utambuzi linaloonyesha uwezo na urazini wala si silika bali ni jambo lililofikiriwa kwa umakini.

Riwaya zimeifananisha kazi ya mtunzi na msukumo uliosanwa kwa njia ya kipekee. Aidha, zoezi la uandishi kama sanaa hufanywa kwa uangalifu (Malenya, 2012). Msimulizi katika riwaya za kisasa husika anapendekeza kwamba riwaya zenyewe zisipuuziliwe mbali kwa madai kwamba muundo wake umekiuka ukawaida. Ni riwaya zilizosanwa na kufumwa kwa njia ya kipekee. Kwa mujibu wa msimulizi katika riwaya teule, ukamilifu wa riwaya hutokea baada ya muda mrefu sawa tu na jinsi msanii anavyochukua muda wake kutengeneza vitu kwa umakini huku matumaini yake daima yakiwa ni kuwavutia wapokeaji wake.

Riwaya zinaendelea kufafanua kuwa mtunzi anapopata msukumo na wazo la kuandika lazima ajiandae vilivyo kupanga hoja, mbinu za lugha na nadharia ya utunzi ili ziambatane na wazo lake

kwani ni zoezi linalochukua muda mrefu. Mtunzi huandika kutokana na msururu mrefu wa vidondoa vingi vyenye misingi ya kitamaduni isiyohesabika. Barry (2009) akimnukuu Barthes amedadavua kuwa matini bunifu si sentensi moja ya maneno yanayowasilisha maana moja inayofahamika na kila msomaji bali ni uwasilishaji wa mawazo mengi yasiyo asilia mengine yakipatana huku mengine yakikinzana. Katika misingi hii riwaya zimebaini kuwa mtunzi *"husana"* kazi yake kwa ubunifu mkubwa. Usanii humfanya mtunzi kubuni kazi yake kwa umakini huku akilenga kuiweka katika kiwango kinachozidi ukawaida mithili ya mbegu ya haradali. Hata ingawa kwa wahariri na wachapishaji mwanzo wa uandishi huonekana kama uvumi, mwisho wake huwa fanaka kwa sababu ya subira ya mtunzi. Hadithi ya Shakespeare inayohusu haradali imerejelewa katika riwaya ili kuelezea ukweli huu. Haradali ni mbegu ndogo sana ambayo inapopandwa na kuota huchukua muda mrefu kukua lakini baadaye huwa mti mkubwa. Mti huo unapozaa, mbegu zake hutumika kukipa chakula chenye ladha nzuri. Aidha, mti huo huwa makao ya ndege wengi. Haradali ya ubunifu imetumika kuashiria subira katika ubunifu ambao matokeo yake huwafaidi wote msomaji na mchapishaji wakiwemo. Kwa mujibu wa riwaya teule mtunzi hutumia mambo madogomadogo katika jamii ambayo mara nyingi huanza kama uvumi ili kujenga ubunifu wake. Hatimaye subira na ukomavu huzaliwa kama inavyodhihirika katika riwaya ya MMM:

> Kwamba katika kiini cha kimbunga cha uvumi kuna haradali ya ubunifu. Ni kama kilele cha wimbi ambacho alisema Shakespeare kuwa kuna ufanisi.**(MMM UK. 19)**

Hata hivyo, riwaya zimekiri ukweli kwamba ubunifu wa kisasa umekiuka ukawaida. Ingawa ubunifu hutokana na msukumo wa ndani wa hisia za mtunzi, kwa msomaji kufahamu yatokanayo na msukumo wenyewe, ni sharti atambue kwamba uandishi wa kisasa umesanwa kwa njia changamano. Uandishi changamano unahitaji ufahamu wa mambo mengi kiada ili ufasirike. Hii ni kwa sababu ujumbe ukusudiwao haujitokezi waziwazi. Makala haya yamebaini kwamba licha ya ukweli kuwa riwaya za kimajaribio zimetokana na msukumo mzito wa hisia za mtunzi, utunzi wenyewe umewasilishwa kwa njia zisizoeleweka. Kwa mujibu wa riwaya mtunzi wa kisasa anafaa kuchunguza uwezo na kiwango chake cha ubunifu ili ajiepushe na fedheha ya uandishi wa kubabaisha. Kazi ambayo haikufanyiwa uchunguzi wa kiada inalinganishwa na mganga anayerogonya tu. Riwaya ya MMM inatuambia:

> "…waandishi wengi hawana uelewa wa kina wa masuala na nadharia ya fasihi. Wanachokuwa nacho ni huo mdadi unaowajia na kuwapa raghba na kuwafanya waandike kazi huku wametwaliwa na nguvu za ajabu, tena wengi wanasombwa tu na kimbunga cha mdadi kama mganga anayepandwa na mdadi na kuanza kurogonya na kuandika tu mambo wasiyoyajua vizuri."**(MMM. Uk.18)**

Riwaya inapendekeza kuwa kila mtunzi anafaa kuandika kuhusu yale anayoyafahamu vizuri na iwapo sivyo, atafute uongozi wa nadharia katika utekelezaji wa wajibu wake. Msimulizi anajaribu kueleza kuwa uandishi wa kijazba usioegemezwa kwenye nadharia hautakuwa na muwala. Uandishi wa kijazba, kama anavyosema msimulizi huwa bora unapoegemezwa katika nadharia maalum ya fasihi. mtunzi anapoongozwa na nadharia ya utunzi hujibana katika kutunga kazi yenye wigo bunifu ikizingatia maisha ya binadamu. Badala ya kurogonya nadharia itamwongoza msanii kubuni kazi yenye ujumbe mzito itakayowasilishwa katika lugha inayosadikika. Kwa mujibu wa riwaya nadharia ni kifaa bora cha kumwongoza mtunzi katika kugusa hisia za ndani ya nafsi za hadhira lengwa.

Isitoshe, riwaya zimebaini kwamba uandishi bunifu hutokana na umaizi, ufunuo, mvuto na uwezo wa kuathiri. Maoni haya yanawiana na yale ya Roland Barthes katika Mike na Gane (2004) wanapodai kuwa uandishi wowote hutarajiwa kuathiri hadhira na kutoa taswira kamili ya jamii yake. Katika riwaya teule msimulizi anatoa ufunuo kuhusu uandishi wa kisasa kwamba si swala la kujipatia pato pekee bali ni jambo lililofikiriwa na kupangwa kwa umakini mwingi. Isitoshe, si kila uandishi uliopo una uwezo wa kuiathiri jamii. Kwa minajili ya haya kuna umuhimu wa kuchunguza kile kinachopelekea kuwepo kwa aina za uandishi usio na mvuto wa kuiathiri jamii kama inavyokusudiwa katika fasihi. Msimulizi anaonyesha kuwa uandishi usiotokana na ujuzi, umahiri na msukumo wa ndani humotishwa na swala la kiuchumi hasa katika kizazi hiki cha Karne ya Ishirini na Moja ambapo

kila mja huwa mbioni kutafuta pesa. Ajabu ni kuwa huu ndio uandishi unaokubalika machoni pa wasomaji, wahakiki, wahariri na wachapishaji. Kinyume na matakwa ya mchapishaji, riwaya zimesema kuwa mtunzi hupata msukumo wa kuandika kutokanana na watu anaoingiliana nao. Kwa hivyo kama mwanajamii, mtunzi husoma kwa mapana na marefu na kufanya utafiti wa kina kuhusu yale anayokusudia kuandika kuhusu jamii yake. Mintarafu ya riwaya za kisasa, ufahamu wa kina wa jamii, matumizi ya nadharia na utafiti hukamilisha tajriba ya uandishi bunifu.

Riwaya zimeongeza kuwa utafiti ni nguzo kuu ya uandishi bunifu. Mtunzi bunifu anafaa kusoma ili kufanya utafiti kuhusu maswala mbalimbali kama vile dini, uongozi na historia kabla ya kuanza zoezi la uandishi bunifu. Hivyo, hawezi kutunga riwaya kabla ya kufanya utafiti wa kina kuhusu jamii anamoandikia. Usomaji wa mapana na marefu ukiambatana na utafiti utamwelekeza mtunzi kwenye uteuzi wa mbinu za lugha na sanaa ili kuwasilisha taswira kamili ya jamii jinsi aionavyo. Nadharia pamoja na utafiti ni mambo mawili yasiyotenganiswha katika uandishi bunifu. Matokeo yake ni uandishi uliopangwa kwa utaratibu na ustadi. Makala haya yameafikia kuwa kila mtunzi mwenye shauku ya kuathiri jamii kupitia kwa ubunifu wake ana shuruti ya kubukua vitabu vingi. Kwa kutumia riwaya, Msimulizi anapendekeza kuwe na matumizi bora ya maktaba zilizomo kwa minajili ya kupata ufahamu na kunufaisha akili.

**Changamoto za Uandishi Bunifu wa Kisasa na Mapendekezo kwa Wasomaji, Wahariri na Wachapishaji**

Sehemu hii imeshughulikia baadhi ya changamoto anazokumbana nazo mtunzi wa riwaya mpya kama ilivyoelezwa katika riwaya zenyewe. Makala imeonyesha jinsi kando na uandishi kuwa mwito wa kipekee wenye kuibua hisia kali, ukamilishaji wake u mikononi mwa wahariri na wachapishaji. Mintarafu ya haya, sehemu hii imefafanua jinsi juhudi za mtunzi zinavyolemazwa na shauku yake kukatizwa na washikadau wenzake, yaani mhariri na mchapishaji. Sehemu hii imetambulisha na kunakili chanzo cha matatizo anayopata mtunzi baada ya kuwasilisha mswada wake, visababishi vya matatizo hayo na jinsi anavyokabiliana nayo. Aidha, mapendekezo kuhusu uandishi, usomaji na uchapishaji bora kama yalivyowasilishwa katika riwaya teule yamefafanuliwa.

**Changamoto za Mwandishi wa Kisasa na Uandishi Bunifu wa Kisasa kwa Jumla**

Sehemu hii inaeleza kwa upana matatizo ya uandishi wa riwaya mpya kama yalivyonakiliwa katika riwaya husika. Riwaya zimeziwasilisha changamoto hizo kwa kutumia mbinu tofauti tofauti za kimajaribio. Simulizi fupi zimetumika kufahamisha kwamba mwandishi hukumbwa na tatizo la ugumu wa kufanya utafiti wa kiada kutoka maktabani kwa sababu ya ukosefu wa vitabu vinavyofaa. Fauka ya hayo, riwaya zimebaini kuwa uandishi unaoathiri ubunifu kisawasawa unahitaji kufanyiwa utafiti kiada tena kwa kina. Kwa hivyo mtunzi husika hana budi kubukua vitabu vingi kama ilivyotajwa awali katika makala. Riwaya zimesema kuwa vitabu vilivyomo maktabani na makavazini havitoshelezi shauku hii. Aidha, idhini ya kuvipata haipo ila kwa "kujuana" kama inavyodaiwa hapa:

> Tangu siku nyingi akitamani kujuana na mfanyikazi wa pale kwa ajili ya utafiti wake kuhusiana na uandishi wake. Alijua fika kuwa vitabu na maandiko yote yaliyopigwa marufuku yalipatikana katika jumba hili. Palikuwa na maktaba ndogo kwenye jengo hilo iliyojaa tungo za wasifu wa kiongozi wa nchi na tafsiri za hadithi nyingi za kizamani kutoka Ulaya, visasili vya Uyunani na mashairi ya Ki-Urdu. Palikuwa pia na matokeo mbalimbali na ya zamani ya tafsiri za Biblia. Lakini ajabu ya ajabu: hapakuwa na kitabu hata kimoja cha Historia! **(ML. UK.65)**

Kwa mujibu wa msimulizi wa *Musaleo!* makavazi na maktaba yaliyopo yamejaa maandishi kutoka Ughaibuni. Inatarajiwa kwamba katika maktaba na makavazi ya nchi kuwe na vitabu vinavyohusu historia za nchi husika. Kinyume na haya maktabani hakukuwa na kitabu hata kimoja cha historia ya taifa. Mtu yeyote akivihitaji vitabu vilivyokuwepo ingawa havikumfaa hana budi "kujuana" na mfanyikazi mmoja maktabani. Ni kinaya kuwa lazima kuwe na "hali ya kujuana" ili kuvifikia vitabu vilivyo maktabani kwani maktaba inafaa kuwa wazi kwa kila atakaye kuitumia. Swali analojiuliza mwandishi ni, "mbona iwe rahisi kupata maandishi kuhusu historia ya nchi nyingine ilhali

isiwezekane kupata ya historia ya mwenyeji?" mtunzi anapoitunga kazi yake anahitajika kuwa na ufahamu wa mazingira anamoandikia, jambo ambalo maktaba zilizomo hazina uwezo wa kulifanikisha.

Mtunzi wa riwaya mpya aidha anakumbwa na changamoto ya kukataliwa na msomaji. Hali ya kukataliwa inadhihirika katika ripoti ya mhariri. Riwaya imewasilisha changamoto hii kwa kutumia mbinu ya dayolojia baina ya mwandishi, msomaji na mchapishaji. Baada ya mtunzi kuikamilisha hadithi yake, anawasilisha mswada kwa mhariri kwa minajili ya kukaguliwa na kutolewa idhini ya uchapishaji. msomaji na mchapishaji kwa pamoja wanaandaa kikao cha kujadili mustakabali wa mswada ambapo mwandishi anaalikwa ili autetee. Changamoto iliyopo ni kwamba msomaji ambaye ndiye mhariri ameshasoma mswada wenyewe na akashindwa kuuelewa. Kauli yake kwa mchapishaji inakuwa kwamba riwaya haingeweza kuchapishwa kwa madai kuwa haikuwa ya kawaida kwani mtindo na muundo wake ulikiuka uhalisia. Maneno ya mwisho ya msomaji yaliyomtamausha mwandishi ni:

> Kauli ya mwisho: haichapishiki! **(MMM. UK.3)**

Kupitia dayolojia hii riwaya zimebaini kwamba mwandishi wa kisasa hudhulumiwa na mhariri na mchapishaji. Ni kinaya kuona kwamba juhudi zote za mwandishi zinaelekea kukomeshwa na mhariri mmoja tu! Mchapishaji anayategemea maoni ya mhariri ambaye tayari ameshaiambatanisha kazi ya fasihi na mwandishi, jambo ambalo Barthes (1968) anapinga kwa kusema; kuimbatanisha kazi ya fasihi na mwandishi ni kupunguza makali yake. Kwa upande mwingine madai ya mhariri ya kuutupilia mbali mswada wa mwandishi ni tetezi kuwa mtindo na muundo wake haukuwa wa kawaida hivyo riwaya ingekuwa tata na changamano kwa wasomaji. Sababu hizi zinatofautiana na maoni ya Fish (1972) anayedai kwamba uchunguzi na ukubalifu kamili wa kazi ya fasihi hauwi mikononi mwa mwandishi bali u mikononi mwa hadhira. Barthes (1968) anaendeleza mjadala huu kwa kupendekeza kwamba ili kuipa uhuru kazi ya fasihi ni sharti msomaji aitenganishe na mwandishi na aitazame kama kazi mahususi ya fasihi. Ili kuepuka ufasiri uliojawa na utawala wa mtu mmoja (Graham, 2003) mhariri na mchapishaji wamtendee haki mwandishi kwa kuichapisha kazi yake ili hadhira ipate nafasi yake ya kufanya uamuzi kuhusu yaliyomo pamoja na ubora wake. Fish (1972) anaongeza kuwa hadhira ndiyo mstahiki dhanifu katika uchunguzi wa kifasihi. Kwa misingi hii, mwandishi anatoa taswira kwamba hadhira kama watumiaji wa fasihi haina budi kuchukua nafasi yake ya kuifanyia riwaya uchunguzi na uhakiki. Thamani ya riwaya inapatikana kwa hadhira. Hapa riwaya zinaonyesha uzembe wa mhariri kama kikwazo kwa uandishi bunifu. Haitoshi kusema kuwa riwaya ina mtindo usio wa kawaida kwani kwa mujibu wa riwaya, huku ni kuikosesha thamani kazi ya mwandishi kama inavyothibitishwa hapa:

> "…jinsi wasomaji na wachapishaji wanavyokosa kuithamini riwaya ya mwandishi kwa kuwa wao wenyewe hawaielewi…"**(MMM. UK. 2).**

Ingawa matumizi ya miundo na mitindo isiyozoeleka huwafanya wachapishaji kupuuza riwaya za kisasa na hatimaye kuiangamiza ari ya mwandishi, kwa upande mwingine mwandishi mwenyewe hujiangamiza (Gallop, 2011). Aidha, dhana ya "kifo cha mwandishi" inayochangiwa na Barthes (1968) inashikilia kuwa panapotokea mwachano baina ya mwandishi na hadhira yake kwa sababu ya ukosefu wa uhalisia katika uandishi, mwandishi husika huua taaluma yake. Mintarafu ya haya mwandishi ajitwike mzigo wa kukataliwa kwa kazi yake wala si kwa sababu ya msomaji. Kwa mfano katika riwaya teule, mwandishi anafahamu fika kuwa riwaya yake haikuwa imeandikwa katika mtindo uliozoeleka na ingekuwa vigumu mswada wake kuchapishwa haraka. Kwa haya, mwandishi anajiangamiza mwenyewe. Riwayani anasema kuwa alitamani sana kuyasikia maoni ya mhariri kama vile mama mjamzito atamanivyo kuona mwisho wa mimba yenye usumbufu mkubwa. Tunaelezwa:

> Ikiwa kuna muswada wa riwaya ambao alitaka kuyasikia maoni ya msomaji ni huu. Mimba ya kuzaliwa kwake ilikuwa na usumbufu mkubwa na kama mjamzito mwenye himila ya aina hiyo anayetaka kuona mwisho wake, alitamani kuona mwisho wake nini. **(MMM. UK.3)**

Taashira hii inabaini changamoto ya jinsi mwandishi anavyobaki katika safari ndefu ya kusubiri uchapishaji wa kazi yake. Tumaini lake likiwa ufahamu kwamba hata ingawa 'mimba' yaweza kuwa ya usumbufu, mwisho wake huwa bora kuliko mwanzo. Mtoto anapopakatwa furaha inayohanikiza humsahaulisha mama na wahusika wengine taabu na matatizo waliyoyapitia. Vivyo hivyo, ingawa uandishi na uchapishaji wa riwaya unachukua muda mrefu na kukumbwa na changamoto tele, mwisho wake ambao ni chapa ya riwaya yenyewe ndiyo furaha ya mtunzi. mwandishi huhisi vyema baada ya kuishika riwaya yake mkononi inapochapishwa. Akiirejelea kauli ya mwanafalsafa Roland Barthes, Jonathan (2002) anasema kwamba ni wakati kama huo ambapo mtunzi pamoja na kazi yake huzaliwa kwa wakati mmoja. Riwaya zinatoa suluhu ya tatizo hili kuwa mwandishi akuze kipawa chake cha uvumilivu na subira ambayo hatima yake ni heri. Mintarafu ya haya ni dhahiri kuwa ufanisi wa uandishi bunifu unapatikana palipo na uvumilivu, bidii na subira. Mwandishi anawasilisha fanaka yake kwa uzungumzi nafsia kwamba:

> Jitayarishe naja mimi hadithi uliyenitafuta, labda utajua mwishowe au nitakueleza baada ya safari ndefu kwenye makaratasi haya. Haya jiandae.**(ML. UK.2)**

Dhuluma kwa mwandishi inazidi kuenezwa na ubinafsi wa wahariri na wachapishaji. Riwaya zimebaini hali hii kwa kufafanua kwamba wachapishaji wanajali maslahi yao ya jinsi watakavyopokea mifedha mingi wakiuza machapisho ya kazi za fasihi kwa wingi. Dhima yao kuu ni mauzo wala si kumkuza mwandishi. Ubinafsi, ubahili na udanganyifu katika sekta ya uchapishaji ni vitendo ambavyo vimeendeleza pakubwa kifo cha mwandishi wa kisasa kulingana na riwaya. Wachapishaji wanaupa kipaumbele ubunifu unaowapa faida kubwa tena kwa haraka. Hatimaye, maslahi ya waandishi wanaotoa jasho jingi katika mradi mzima wa uandishi na uchapishaji yanapuuziliwa mbali. Hali hii ya ubinafsi inadhihirika katika dayolojia hii:

> "Upitie haraka haraka…unaweza hata kufanya *skip reading* hapa na pale lakini hakikisha udhaifu wake unatawala. Amekuwa king'ang'anizi mno."**(MMM UK. 103).**

Dhana ya "kuwa king'ang'anizi" inatoa taswira kwamba wachapishaji wanawaona waandishi wa riwaya za kisasa wakiwa wasumbufu badala ya kuwaona kama watu wenye hima na bidii ya kutimiza ndoto zao za ubunifu. Ili kuuzima usumbufu huo, wachapishaji wanawatumia wahariri kwa kuwaelekeza kwamba wakishasoma miswada kauli iwe moja, "haichapishiki". Katika dondoo hili ubinafsi wa wachapishaji unadhihirika pindi msomaji anapopendekeza kwamba, "ni hadithi isiyo ya kawaida hasa kwa wasomaji wetu, ifanyiwe *skip reading*" yaani isomwe haraka haraka na ripoti ikitolewa ionyeshe kazi yenye dosari nyingi. Katika riwaya ya *Mwandishi, Msomaji na Mchapishaji* mhariri anafafanua tamaa na ubinafsi katika vitengo vya uhariri na uchapishaji zaidi anaposema:

> "Ni hadithi isiyokuwa ya kawaida…" hasa kwa wasomaji wetu eh…ehh..ehhh!" akachekacheka kabla ya kuendelea, " wajua soko letu kubwa ni shuleni bwana, huko nje hakuna atakaye kusoma, ni wasomaji wetu wachache tulio nao bwana, wanapenda njia walizozizoea. "Eh wasomaji wanaweza kushtuliwa na wasichokizoea." **(MMM UK. 16)**

Taaluma ya uandishi inafikwa na msiba mwingine pale Msimulizi anapoonyesha waziwazi namna wachapishaji wanavyothamini mauzo ya vitabu vya fasihi na faida watakayopata kutokana na mauzo hayo bila kuzingatia utendakazi wa vitabu hivyo kwa hadhira. Eagleton (2008) anaonyesha dhima moja ya fasihi kwamba ni kuwafanya wapokeaji wake kuzifikia hisia zilizo vilindini mwa mioyo kuhusu tabia za watu ambazo hazingesemwa kadamnasi. Vilevile, fasihi hutumika kufunzia lugha kwa sababu ya kuwepo kwa tamaduni mbalimbali ndani yake (Damon et al., 2006). Damon na wenzake wanaendelea kufafanua kuwa kuwepo kwa maswala ya kitamaduni katika fasihi hukuza mbinu za ujifunzaji lugha kwani lugha yenyewe ni sehemu ya utamaduni. Kando na haya, fasihi humkuza msomaji kisaikolojia na kumpa uelewa wa hisia zinazompa hofu (Hogan, 2011). Zaidi ya yote dhima ya fasihi ni burudani na kuwafaidi wajumi kwa kuwapa umaizi wa maoni ya mwandishi kuhusu hali mbalimbali za kibinadamu (Lombardi, 2020). Maoni haya kuhusu majukumu na dhima ya fasihi yanatofautiana na ya mchapishaji anayemchukulia mwandishi kama mzizi wake wa utajiri. Kwake fasihi ni kitega uchumi, jambo linalomwangamiza mwandishi.

Hali kwamba wachapishaji wa riwaya hawana haja ya kuchapisha kazi zinazouzika shuleni pekee ni kinyume na dhima ya fasihi. Hili ni pigo kubwa kwa uandishi wa riwaya mpya na ukuzaji wa kazi za fasihi kwa jumla. Hali hii inazidi kufunua ubinafsi wa wahariri na wachapishaji waziwazi kwamba hamu yao kubwa ni kuzalisha faida wala si kueneza ufahamu na kumkuza mwandishi. Kando na haya, riwaya zinabaini kwamba wasomaji waliopo hawako tayari kupokea kazi tofauti kifani huku wachapishaji wakitegemea shule kama soko kuu. Haya yanaibua taswira mpya miongoni mwa jamii kwamba wapokeaji wa fasihi ni wanafunzi labda kwa minajili ya kufaulu katika mitihani. Katika kutatua tatizo hili mwandishi kama mwanajamii anamtaka kila mmoja katika jamii awe msomaji na mpokeaji wa kazi za fasihi. Hata ingawa wanajamii hawapendi kuondoka kwenye mitindo waliyoizoea riwaya zimependekeza kuwa kukumbatia riwaya za kisasa zenye fani zisizozoeleka ni sawa na kupanua mawazo.

Hakuna riwaya yoyote iliyo kamilifu, riwaya zote hukamilishwa na wasomaji. Ni jukumu la kila msomaji kuikamilisha riwaya kwa kujaliza mapengo yalioachwa na mwandishi. Hivyo, lalama kwamba hadithi kamilifu pekee ndizo zinazofaa kuchapishwa hazina mashiko. Ni wajibu wa wahariri na wachapishaji kusoma na kuchapisha riwaya kutoka kwa waandishi ili kuipa hadhira nafasi ya kupanua ufahamu na ujuzi wao wanapojaza mapengo yaliyoachwa. Mintarafu ya haya wasomaji wote wanafaa kujilia na kujitafunia chakula walichoandaliwa na mwandishi kama inavyodhihirika hapa:

> Kwa kifupi tuseme hivi…hakuna hadithi yoyote inayosimuliwa katika ukamilifu wake…kila hadithi huwa na mapengo fulani? Hata hii ina mapengo? Akauliza Mchapishaji. Hii ni hadithi pia! Sasa hayo basi ndiyo tunapaswa kuyazungumzia. **(MMM UK.19)**

Tunajuzwa kwamba hadithi ni matokeo ya kazi ya mwandishi na ina haki ya kupewa nafasi ya kuifikia hadhira. Dhana hii inatetewa na William Shakespeare katika mojawapo ya semi zake kama ilivyorekodiwa katika tamthilia yake ya *Henry VI* anapodokeza kuwa kazi ya mwandishi ni kuchukua kalamu na wino na kuandika yaliyo akilini mwake (Dobson, 1995). Isitoshe, mwandishi hubuni kazi mahiri ambamo hueleza mambo jinsi ayaonavyo japo kwa kutumia uchangamano wa hali ya juu. Riwaya zimewiana na Paris (1986) kwamba uchangamano katika ubunifu wa fasihi ni sharti uwepo kwa maana lugha ya fasihi ni ya kitamathali au kiistiari.

**Mapendekezo Kuhusu Uandishi na Uchapishaji wa Riwaya Mpya**

Sehemu hii inatoa mapendekezo ya kukuza uandishi bunifu wa riwaya za kisasa kama yanavyoakisiwa katika riwaya teule. Licha ya changamoto anazopitia mwandishi wa riwaya mpya, kuna matumaini kwamba uandishi bunifu wa riwaya mpya unaweza kufaulu, kukua na kuendelea mbele. Inakisiwa kuwa iwapo washikadau wote watayakumbatia mapendekezo yaliyodokezwa na riwaya huenda kwa kiasi fulani uandishi bunifu na uchapishaji hasa wa riwaya za kisasa ukapata nguvu na sura mpya. Mapendekezo hayo yanaelekezwa kwa mwandishi, msomaji na mchapishaji. Japo riwaya zimefafanua changamoto si haba katika uandishi, uhariri na uchapishaji wa riwaya mpya, riwaya zenyewe zimependekeza mbinu mbalimbali kwa mwandishi, msomaji na mchapishaji za kutoa uandishi kwenye matatizo hayo.

Kuhusu mwandishi, riwaya zimempendekeza kuwa japo uandishi ni kariha yenye mwito wa kipekee huchukua muda mrefu kwani ni sharti kazi ipangwe hatua kwa hatua. Kwa mujibu wa riwaya utaratibu ufuatao unakisiwa kumwelekeza mwandishi ifaavyo. Jambo la kwanza, kama mwanajamii, mwandishi atahitaji kufanya utafiti ili kujaliza kikamilifu mapengo ya kiusomi yaliyomo katika jamii anamoandikia. Pia, utafiti ni njia bora ya kutatua matatizo yanayoikabili jamii. Uandishi unaofaulu na wenye mnato hujiri baada ya kusoma kwa mapana na marefu kama inavyoelezwa katika *Musaleo!*

> Alivipitia vitabu alivyovipata na kuandikaandika madondoo fulani kwenye kidaftari chake cha kukusanyia mawazo anayoyatumia aandikapo. Kingunge alikuwa amebukua vya kutosha na kupata mawazo mengi aliyoyataka.**(ML. UK.65)**

Riwaya zimemtaka mwandishi yeyote wa kazi za fasihi ajiepushe na mwenendo wa kijadi wa kuchapisha kazi ambazo hazijatafitiwa kwa kina. Ili kutimiza haya waandishi watarajiwa wanatazamiwa wazitumie maktaba zilizomo kwa manufaa ya kazi zao. Habari zote ziwe za siasa, dini,

uchumi, mahusiano, lugha na nadharia hupatikana maktabani na huwa vijenzi muhimu vya uandishi bunifu. Zaidi ya hayo, utaratibu wa utafiti pia ni hatua ya kimsingi muhimu katika uandishi bunifu. Hatua hii imezungumziwa kwa kirefu katika riwaya zilizotumika katika makala hii. Mintarafu ya haya, uandishi utakaofaulu na wenye mnato huafikiwa baada ya kusoma.

Msimulizi katika *Musaleo!* anazidi kumdokezea mwandishi namna ya kuandika fasihi bora ilyokomaa baada ya kufanyiwa utafiti. Kwa kutumia simulizi fupi, riwaya zimeonya dhidi ya tabia za waandishi wengine ambao wanahusudu matumizi ya njia za mkato katika shughuli zao. Ili jambo lolote lifaulu lazima mikakati na utaratibu uliowekwa ufuatwe kikamilifu tena kwa ustadi. Kwa mujibu wa haya ni sharti kila mwandishi aliye na shauku ya kuiathiri jamii kupitia kwa uandishi atimize masharti yote yaliyopendekezwa katika riwaya kuhusu utunzi bora; kusoma na kutafiti. Katika kitengo cha kusoma, imependekezwa kwamba msomaji anukuu na kuhifadhi aliyoyasoma katika vijidaftari ili yasisahaulike. Aidha, katika kuhakikisha kuwa mpango na ratiba bora imefuatwa kikamilifu, kila mtunzi ajiwekee makataa ya kazi yake na kuifuata bila kusita. Katika safari ya utunzi kutakuwa na panda-shuka mbalimbali lakini waandishi wanahimizwa kuwa la muhimu ni uamuzi watakaoufanya wenyewe. Dondoo lifuatalo linaweka wazi ukweli huu:

> Alipofika nyumbani aliamua kuiendeleza hadithi yake ambayo sasa kapania kuimaliza baada ya kushindwa kuimaliza wakati aliotarajia. **(ML. UK.66).**

Vilevile, riwaya zimebaini kwamba kila mtunzi ni sharti awe na nidhamu na msukumo wa kipekee ili aikamilishe kazi yake kwa wakati ufaao. Msimulizi ametumia mfano wake mwenyewe kuonyesha jinsi alivyofaulu katika mradi wake wa uandishi wa riwaya mpya ya *Musaleo!* katika simulizi fupi hii:

> Hadithi yangu nimekuwa nikiisimulia kwa miaka mingi. Utangulizi wake ulichukua miaka kama kumi kumaliza. Mwanzo hadhira yangu ilikuwa ndogo. Niliposema paukwa tu wengine waliondoka kwenda kujiandalia sherehe za kusherehekea matamu ya ukombozi. Waliobakia walikuwa wachache wengi wao wakulima, wanafunzi waliokuwa wakifanya utafiti pamoja na mwalimu wao (huyu Profesa), watoto wanaopenda hadithi. Watu walianza kurudi mmoja mmoja baadaye nilipokuwa nimejibiwa pakawa na wachache waliokuwako. **(ML. UK.72)**

Muda mrefu katika zoezi la utunzi husababisha kazi bora iliyofumwa kwa ustadi. Ubora wa kazi hii hujidhihirisha kwa hadhira mahususi ya wasomaji walioongoka na ambao pia ni watafiti. Aidha, kazi husika hukumbatiwa na wasomaji chipukizi wanaopenda kuisoma kwa minajili ya kujifurahisha. Polepole, idadi ndogo ya wasomaji hujengwa na kwa mujibu wa mpito wa wakati kazi hiyo hupata wasomaji zaidi.

Kwa mhariri riwaya zinamkemea dhidi ya uzembe katika zoezi la usomaji kama unavyowakilishwa riwayani na msomaji. Riwaya zinahimiza haya katika nukuu hili:

> "usikiapo lolote lipindue uangalie kama kinyume chake kinaweza kuwa na maana mbaya" **(ML. UK. 10)**

Kulipindua na kuliangalia jambo kunakorejelewa ni kulichunguza kwa makini. Uchunguzi wa kindani unapofanywa majawabu hupatikana. Kwa mujibu wa haya, usomaji wa riwaya usiwe wa juujuu bali uwe na nia ya kuchunguza kile mwandishi anachotaka kuifahamaisha jamii. Kuchunguza kwa undani ni njia moja ya kujaliza mapengo yaliyoachwa na mwandishi kama ilivyoelezwa awali. Aidha, ni mbinu ya kufanya utafiti ambao mwishowe huleta majibu yanayoifaa jamii. Utafiti kama njia bora ya kutatua matatizo yanayoikabili jamii utapunguza hali ya uzembe wa kusoma iliyokithiri katika jamii ya kisasa. Kwa mujibu wa riwaya, mbinu mojawapo ya kukabiliana na uzembe wa usomaji ni kuwasilisha hadithi isiyo ya kawaida. Usomaji wa kazi za uhalisia zilizozoeleka na zinazowasilishwa kwa njia ya moja kwa moja unasababisha uzembe kwa sababu mapengo yote yamezibwa. Hamu kubwa ya mwandishi ni kuikuza hadhira. Kwa sababu hii riwaya zinahimiza hadhira kuacha kuwategemea wahakiki kila uchao kwa minajili ya kuifafanulia hadithi. Japo kazi za kisasa zinawakanganya na kuwazungusha wasomaji, uhalisia pekee si suluhu. Mambo yaliyozoeleka hayaongezi maarifa kwani,

> Hii sio dunia ya kuridhika na tulichozoea…" **(ML. UK.55)**

**Hitimisho**

Makala haya yamezingatia mchakato mzima wa uandishi na uchapishaji wa riwaya mpya ya Kiswahili kwa kuangazia pembetatu ya uandishi bunifu iliyofumwa na mwandishi, msomaji na mchapishaji. Kwa mujibu wa riwaya uandishi ni mwito wa kipekee wenye hisia na msukumo usiozuilika. Mwito huu umetimiza hatua mbalimbali kama vile uteuzi wa lugha faafu, uchaguzi mwafaka wa nadharia na utafiti wa kina. Hata hivyo, imedhihirika kuwa kimuundo na kimtindo uandishi wa riwaya ya kisasa umekiuka ujadi uliozoeleka. Kwa sababu hii mwandishi wa kisasa amezua vita kati yake na mhariri na mchapishaji. Vita hivi vinatishia kuiangamiza tajriba ya mwandishi. Vilevile, riwaya zimeangazia uhusiano huo hususan namna jitihada za kiubunifu za mwandishi zinavyokwamizwa na wahusika hao wawili; mhariri na mchapishaji. Hata hivyo, pamoja na changamoto zilizoangaziwa, riwaya zimethibitisha kuwa uandishi bunifu ni zoezi la wateule, si la kila mja. Makala imeng'amua kwamba ili kazi bunifu ya kisasa ikue ni sharti wahariri na wachapishaji wabadilishe mielekeo yao kuhusu waandishi wa kisasa. Vilevile, ni sharti uzembe uliopo miongoni mwa wahariri uondoke na wakubali kuzifanyia riwaya mpya uchunguzi wa ndani ili kuuelewa usanii wake baada ya kubaini yaliyomo. Kuhusu uchapishaji, japo ni kweli kwamba riwaya za kisasa ni changamano na huenda zikakosa kuwapendeza wengi kama asemavyo Rettova (2016), kauli mbiu ni kuwa kazi zote zina haki ya kuchapishwa ili hadhira ipate nafasi ya kutoa uamuzi wake. Hatimaye, makala haya yanahimiza kuwa ufanisi wa riwaya mpya ya Kiswahili utaimarishwa na ushirikiano baina ya washikadau wote watatu yaani; mwandishi, msomaji na mchapishaji.

**Marejeleo**


Barry, P. (2009). *Beginning Theory*. Manchester: Manchester University Press.

Barthes, R. (1968). *The Death of the Author*. 1st ed. University Handout.

Baudrillard, J. (1988). *Selected Writings*. Stanford: Stanford University Press.

Bloom, H. (1996). *Maya Angelou's I know Why the Caged Bird Sings.* New York: Chelsea House Publishers.

Burke, S. (1992). *The Death and Return of the Author: Criticism and Subjectivity in Barthes, Foucault and Derrida.* Edinburgh: Edinburgh University Press.

Burke, S. (1995). *Authorship: From Plato to Postmodern: A Reader*. Edinburgh: Edinburgh University Press.

Damon W., Lerner, R., Renninger, A.na Sigel, I. (2006). *Handbook of Child Psychology: Child Psychology in Practice.* Hoboken: John Wiley and Sons.

Dobson, M.S. (1995). *The Making of the National Poet: Shakespeare, Adaptation and Authorship* 1660-1769. Oxford: Oxford University Press.

Eagleton, T. (2008). *Literary Theory: An Introduction.* Oxford: Blackwell Publishing.

Fish, S.E. (1972). *Self Consuming Artifacts: The Experience of Seventeenth- Century Literature.* California: California University Press.

Freud, S. na Strachey, J. (2010).*The Interpretation of Dreams*. New York: Basic Books.

Gallop, J. (2011). *The Deaths of the Author: Reading and Writing in Time.* Durham: Duke University Press.

Graham, A. (2003). *Roland Barthes*. London: Routledge.

Halliwell, S. (1992). *Teaching English in the Primary Classroom*. London: Longman.

Hogan, P.C. (2011). *What Literature Teaches us About Emotion.* New York: Cambridge University Press.

Jonathan, C. (2002). *Barthes: A Very Short Introduction.* Oxford: Oxford University Press.

Lombardi, E. (2020). *What Literature Can Teach Us*. Retrieved from https://www.thoughtco.com/what-is-literature-740531

Malenya, M.M. (2012). *Matumizi ya Lugha katika Fasihi Simulizi*. Mwanza: Inland Press.

Mike, G. na Gane, N. (2004). *Roland Barthes.* London: SAGE Publications.

Mohamed, S.A. (1995). *Kunga za Nathari ya Kiswahili.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Rettova, A. (2016). Writing in the Swing? Neo-realism in Post- Experimental Swahili Fiction. *Research in African Literatures,* (47) 2, 15-31.

Senkoro, F.E.M.K. (1987). *Fasihi na Jamii*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre. Simiyu, W. F. (2011). *Kitovu cha Fasihi Simulizi*. Mwanza: Serengeti Bookshop.

TUKI. (2015). *Kamusi ya Kiswahili – Kiingereza*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Vernick, L. (2016). *Self-Esteem; Looking Up Instead of Looking in.* Harvest, USA: New Growth Press.

Wamitila, K.W. (2004). *Musaleo!* Nairobi: Vide-Muwa Publishers.

Wamitila, K.W. (2010). *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi.* Nairobi: English Press.

Wamitila, K.W. (2014). *Mwandishi, Msomaji na Mchapishaji.* Nairobi: Vide-Muwa Publishers.

Wilson, A. (2004). Foucault on the Question of the Author: A Critical Exegesis. *The Modern Language Review, 99*(2), 339-363. doi:10.2307/3738750